



Kumb. Na. NDC/I.20/6/ Vol VII/171

Tarehe 28 Nov, 2022

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA WA MUDA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anatangaza **nafasi 2** za kazi za Mkataba wa Muda za **Afisa Ugavi daraja II**, Hivyo, anakaribisha maombi kwa watazania wote wenye sifa na uwezo, kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi kama ilivyo orodheshwa katika tangazo hili. Aidha mnajulishwa kuwa mwisho wa maombi haya ni tarehe **08/12/2022**.

### 1. AFISA UGAVI DRJ II - NAFASI 2.

#### a) Sifa za mwombaji.

- I. Mwenye elimu ya kidato cha nne au sita,
- II. Shahada ya Biashara yenye Mchepuo wa Ugavi, Shahada ya Ugavi au Stashahada ya Juu ya Ugavi.
- III. Stashahada katika "National Material Management" au "Professional Stage II"

#### Kazi na majukumu

- (i) Kuandaa mpango wa manunuzi wa mwaka;
- (ii) Kushauri kuhusu masuala yanayohusu manunuzi ya bidhaa na huduma na usimamizi wa vifaa katika Halmashauri;
- (iii) Kuratibu manunuzi ya bidhaa, huduma na usimamizi wa usafirishaji;
- (iv) Kupata mali, Rejesta ya Kusasisha na inahakikisha kwamba mali zimewekewa kanuni ipasavyo;
- (v) Kununua, kudumisha na kusimamia vifaa, nyenzo na huduma ili kusaidia mahitaji ya vifaa;
- (vi) Kudumisha na kusasisha orodha ya bidhaa, vifaa na nyenzo;
- (vii) Kutayarisha nyaraka za zabuni na kutangaza fursa za zabuni;

(viii) Kutayarisha nyaraka za mkataba; na Kutoa huduma za sekretarieti kwa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri).

Atawajibika kwa Mkuu wa Kitengo cha huduma ya Manunuzi na kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Njombe .

## 2. MAELEKEZO

- i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania ambao hawazidi umri zaidi ya miaka 45 na hawapungui umri wa miaka 18.
- ii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya **TANGAZO LA KAZI**,
- iii. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
  - a) Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita.
  - b) Cheti cha Taaluma
  - c) Cheti cha kuzaliwa.
  - d) Picha mbili za passport size.
- iv. Hati ya matokeo ya kidato cha nne/sita (Result slip) haitafanyiwa kazi.
- v. Wenye Uzoefu usiopungua mwaka mmoja kwenye kazi za Kitengo cha Manunuzi watapewa kipaombe.
- vi. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kingereza.
- vii. Watakoitwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe.
- viii. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 08/12/2022 saa 9:30 alasiri, baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa na watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri [www.njombedc.go.tz](http://www.njombedc.go.tz) na kwenye mbao za matangazo za Halmashauri.

Barua zote zitumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,  
S.L.P 547,  
**NJOMBE.**

Tangazo hili limetolewa na:-

  
Sharifa Y. Nabalang'anya  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
NJOMBE

**Mkurugenzi Mtendaji**  
**Halmashauri ya Wilaya**  
**NJOMBE**